
www.ippmedia.com

# Alasiri Online

ISSN 0856 Na. 001 Jumamosi Machi 23, 2019 Tanzani 500/-, Kenya 50/-



## ASLAY AIBUKA NA NYANG'ANYANG'A



## TUNDA ADAKA DUME LAKE



## MR BLUE AGOPA MCHEPUKO



# AMBER LULU MKOROGO DAMUDAMU

# AMBER LULU

## MKOROGO DAMUDAMU

Na Mary Kadoke

HUKU wasanii wengine wakikana kutumia mkorogo, muimbaji Amber Lulu amekiri kuutumia na kugharimika pesa nyingi kuifanya ngozi yake kuwa mithili ya mzungu.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online amesema kung'arisha huko ngozi yake huja na tenda nyingine ya kusaka losheni itakayomsaidia kutoa sugu au mbadala wa mkorogo utakaompa matokeo mazuri zaidi ya aliloutumia awali.

"Ndio natumia, rangi nyeupe naipenda nikifikia kama Sara Mzungu wa Harmonize nitafurahi sana nahisi nitakuwa pambe," amesema.

"Mkorogo unanigharimu kwa sababu nanunua mafuta kila parcel Sh 500,000 au Sh 300,000 kwa mwezi, huu ukinikataa inabidi ninunue mwingine so ni kitu ambacho nakipenda," ameongeza.

Muuza nyago Official Nai ni kati ya wasanii waliowahi kudaiwa kutumia mkorogo na baada ya Alasiri Online kumhoji kuhusu tuhuma hizo alisema anang'arishwa na losheni ya kawaida sana inayofanya watu waishie kusema ni mkorogo.



# Aslay aibuka na Nyang'anyang'a

Na Anaeli Mbise

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo fleva Aslay ametambulisha kibao chake kipya cha Nyang'anyang'a mwishoni mwa wiki iliyopita.

Akizungumza na Alasiri Online, meneja wa msanii huyo Chambuso, amesema ujio wa wimbo huo ni mfululizo wa ngoma nyingine kali zinazokuja ambazo ndani yake atawashangaza wengi.

Amesema katika vibao vitatu vitakavyotambulishwa kutawashirikisha wasanii wakali kutoka nje ya nchi na kufanya Aslay kuanza kuvuka mipaka.

"Nyang'anyang'a ni wimbo tulioutambulisha ikifuatiwa na nyimbo nyingine tatu ambazo mtaona kuna mapinduzi makubwa aliyofanya akishirikiana na wanamuziki wa nje," amesema Chambuso.

Hata hivyo, Chambuso amepinga uvumi kwamba Aslay amerudi katika kundi la Yamoto, akisema msanii huyo anaangalia mbele na siyo sehemu alipotoka.

"Mashabiki wasisikilize uongo wa watu, Aslay harudi nyuma ataendelea kusonga mbele," ameongeza kusema.





# CHUCHU AJA NA PLAY BOY

Na Anaeli Mbise

MUIGIZAJI wa Bongo movies Chuchu Hans amerudi tena kazini na safari hii anakuja na filamu inayoitwa 'Play Boy' ambayo amesema ina vitu vingi vipya.

Akizungumza na Alasiri Online, Chuchu amesema tayari wametoka nje kwa ajili ya kuchukua picha za movie hiyo na kusema kuwa muda siyo mrefu ataitambulisha kwa mashabiki.

"Najua mashabiki wa filamu wanataka nini, naamini ndani ya 'Play Boy' kuna mabadiliko mengi ambayo yatawapa furaha kurudisha imani kwa kazi zetu za ndani," amesema Chuchu.

Aidha amesema kuwa ndani ya movie hiyo kutakuwa na vitu kama ndoa za uongo pamoja na mapenzi ya udanganyifu.

Muiugizaji huyo pamoja na shughuli za sanaa pia anafanya ujasiriamali wa kuuza vitu vya urembo pamoja na nguo.

# TUNDA ADAKA DUME LAKE



Na Mary Kadoke

PAMOJA na umaarufu wa muuza nyago 'Video Vixen' Tunda Sebastian, amesema siku si nyingi atawashangaza watu kwa kufunga pingu za maisha na mwanaume asiye na jina kubwa hapa mjini. Amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online na kusisitiza kuwa maamuzi hayo ni baada ya kubahatisha mwanaume anayempenda na kumheshimu tofauti na mahusiano yake ya awali.

"Naolewa soon tena na mwanaume tunayependana na kuelewana na sio kama drama za wengine waliopita," amesema.

"Nimeamua kutulia ili majukumu yaliyo mbele yangu yasije nishinda," ameongeza.

Awali Tunda aliwahi kuwa kwenye mahusiano na muimbaji Young Dee ambaye baada ya kuachana naye alikuwa na mtangazaji Casto Dickson ambaye pia walikuja kuachana.

Kwa mahusiano haya, walengwa wote mpaka leo hawajawa tayari kueleza kilichowakumba mpaka kufikia hatua ya kila mmoja kushika hamsini zake. Video iliyowahi kumuweka Tunda mjini katika biashara yake ya kupamba video ni 'Furaha' ya Young dee.



# Mr Blue agopa mchepuko

Na Mary Kadoke

KATI ya vitu asivyotamani kufanya miongoni mwa manguli wa Bongo Fleva, Mr Blue ni kuzaa nje ya ndoa kwani madhara yake amewahi kuyaishi, hivyo asingependa yatokee kwa watoto wake.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online amesema changamoto iliyopo ni kwamba linapotokea suala kama hilo watoto hukosa malezi ya pande zote mbili.

“Mimi nimelelewa na upande mmoja wa mama, hivyo sikuwa napata malezi ya pande zote mbili,” ameeleza.

“Nilikuwa naona shida sana kwani kama mtoto hupati malezi yanayostahili, ndio maana mimi sitaki ijirudie kwangu,” ameongeza.

Blue aliyefunga ndoa Aprili 2016 na mke wake Waheeda, wamejaaliwa kupata watoto wawili wa kiume Kherry (6) na wa kike Riyah (3).

Kibao chake kinachomuweka bado kwenye chati ni Blue.



# BIZMAN kufyatua kitu

Na Anaeli Mbise

MSANII mwenye vipaji kibao Bizman yuko mbioni kutoa kibao kipya baada ya kuwa kimya kwa muda mrefu.

Akizungumza na Alasiri Online, Bizman ambaye ni mwimbaji, mtayarishaji wa muziki na mcharaza kinanda, amesema mwisho wa mwezi huu atarekodi kibao kipya ambacho kitajulikana kwa jina la Maisha Halisi.

"Kwa sasa ninao muda wa kutosha ambao unanilazimu nitoe nyimbo mpya kuanzia mwishoni mwa mwezi huu ili kuwapa raha mashabiki wangu," amesema Bizman.

Akizungumzia ujumbe unaopatikana katika ngoma hiyo amesema kuwa unazungumzia hali halisi ya maisha ya binadamu katika utendaji wa kazi pamoja na changamoto wanazokumbana nazo katika utafutaji.

Mwanamuziki huyo aliwahi kutamba na ngoma kali kama vile Riziki, Ametoroshwa, Mabinti wa Bongo pamoja na Nishike Mkono.



# Cheka atembeza bakuli

Na Anaeli Mbise

MKONGWE wa Bongo fleva, Bi. Cheka ameweka wazi hali ya afya kuwa siyo nzuri, na kuwa anahitaji msaada wa Watanzania kumudu gharama za matibabu.

Akizungumza na Alasiri Online, Bi. Cheka amesema kwa sasa anasumbuliwa sana na tatizo la moyo, na dawa anazotumia ni ghali, hivyo anaomba msaada ili kuzipata.

Moyo unaenda mbio, mara nyingine nakosa nguvu, kuna tatizo la moyo tu unaniuma, dawa kopo linauzwa laki moja (100,000/-), na linatumika ndani ya miezi miwili, amesema Bi. Cheka.

Hizi dawa zimetoka Ugiriki alikofia mtoto wangu ndiyo marafiki zake wakasema tumchukulie mama ila hapa nimetafuta sana hamna, amesema Bi. Cheka.

Akiendelea kuzungumzia hilo Bi. Cheka amewataka watu hata akifa waende kwa wingi wakaamzike, kwa sababu anawapenda sana.

Mwanamuziki huyo ametamba na ngoma kama vile Nalia, Ni Wewe pamoja na Hali Yangu.